

CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHMBILI

OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO

P.O. Box 65001
DAR ES SALAAM
TANZANIA
Web: www.muhas.ac.tz



Tel G/Line: +255-22-2150302/6 Ext. 1024
Direct Line: +255-22-2151596
Telefax: +255-22-2150465
E-mail: vc@muhas.ac.tz

DOKEZO NA. 1 - 2018

KUTOKA: Makamu Mkuu wa Chuo

KWENDA: 1. Manaibu Wakuu wa Makamu Mkuu wa Chuo
2. Wakuu wa Skuli na Kurugenzi
3. Wakuu wa Idara

TAREHE: 5 Disemba, 2018

YAH: UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MAOMBI MBALIMBALI YA KUSAFIRI NJE YA NCHI

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

Hii ni kuwafahamisha kuwa tumepokea barua kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusiana na ushughulikiaji wa maombi ya kusafiri nje ya nchi ambayo yanafanyika kwa njia ya mtandao (*Online Application*). Imeelezwa kuwa pamoja na ufanisi uliopatikana kwenye matumizi ya mfumo huo, bado zimeendelea kuibuka changamoto mbalimbali kwa waombaji ambazo ni:-

- Waombaji kutofuata maelekezo ya kujaza fomu za maombi
- Waombaji kutoweka taarifa zao kwa uwazi na (hasa zinazohusu gharama za safari) na
- Waombaji kusafiri safari ambazo hazina manufaa kwa Taifa au sisizo wahusu.

Imeelezwa kuwa Changamoto hizi zimekuwa zikichelewesha uidhinishaji wa maombi ya vibali vya safari au kutoidhinishwa kabisa na mamlaka husika. Hivyo basi ili kuendelea kutumia huduma hii kwa ufanisi zaidi imeagizwa kama ifuatavyo:-

- Waombaji wote kufuata maelekezo ya kujaza fomu za maombi kwa ufasaha;
- Waombaji wanaojigharamia kutojaza kiwango cha fedha (kuweka 00) kwenye kipengele cha gharama za safari;
- Waombaji wanaogharamiwa na miradi ya wafadhili ambao fedha hizo sio mkopo unaolipwa na serikali wataje jina la mfadhili kama lilivyo kwenye barua ya mwaliko na (kuweka 00) kwenye kipengele cha gharama za safari;
- Waombaji wanaogharamiwa na serikali wajaze kiasi chote cha fedha kwa kuzingatia miongozo ya malipo ya serikali na;
- Waombaji wanaogharamiwa na miradi ambao fedha hizo ni mkopo unaolipwa na serikali pia wajaze kiasi chote cha fedha kwenye kipengele cha gharama za safari kwa kuzingatia miongozo ya malipo ya serikali;
- Kila kiongozi kusimamia na kuhakikisha kila mtu anasafiri safari inayomhusu na yenye maslahi kwa Taifa.

Imesisitizwa kuwa kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa hasa katika kudhibiti matumizi ya Serikali, fedha za miradi zinazotumika kwa safari za nje ambazo ni za mkopo na serikali itakuja kulipa hivyo ni vyema zikatumika kwa safari muhimu tu.

Kwa Dokezo hili mnatakiwa kuzingatia maagizo ya Serikali na kuwafahamisha wafanyakazi walio chini ya Skuli/Kurugenzi na Idara kuwasilisha maombi yao **kabla ya siku 28 Wizarani na siku 14 kwa Katibu Mkuu Kiongozi** kabla ya safari husika.

Nawatakia utekelezaji mwema.


Prof. Andrea B. Pembe

MAKAMU MKUU WA CHUO

Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili
S. L. P. 65001
Dar es Salaam

/fk